JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2023

## MAARIFA YA JAMII

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2023

# 614 MAARIFA YA JAMII

*Kimechapishwa na:*

Baraza la Mitihani la Tanzania,

S.L.P. 2624,

Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iv
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI .. 1
2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi ........ 1
2.1.1 Swali la 1: Sayari Dunia. ........ 2
2.1.2 Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani ........ 4
2.1.3 Sayari Dunia. ........ 6
2.1.4 Nchi yetu Tanzania ........ 9
2.1.5 Maandalizi ya kufundisha na kujifunza. ........ 11
2.1.6 Swali la 6: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika ........ 14
2.1.7 Swali la 7: Ufundishaji wa Mada za Somo la Historia ........ 17
2.1.8 Swali la 8: Mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika huru. ........ 19
2.1.9 Swali la: 9 Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa KikoloniAfrika ........ 22
2.1.10 Swali la 10: Mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika Huru ........ 24
2.2 Sehemu B: Maswali ya Insha ........ 27
2.2.1 Swali la 11. Sayari Dunia ........ 28
2.2.2 Swali la 12. Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika ........ 33
2.2.3 Swali la 13. Upimaji na Tathmini. ........ 38
2.2.4 Swali la 14. Kujiandaa kwa ajili ya kufundisha ........ 42
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA .. ........ 46
4.0 HITIMISHO ........ 47
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 47
KIAMBATISHO ........ 48

## DIBAJI

Taarifa hii inahusu Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Ualimu Daraja la IIIA uliofanyika Mei 2023 kwa masomo ya Jiografia na Historia ambayo yameunda mtihani wa Maarifa ya Jamii. Lengo la kuandaa taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala na wadau mbalimbali wa elimu, juu ya ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii (GATCE) 2023.

Mitihani ni namna mojawapo ya kupima na kutathmini mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Tathmini hiyo inawezesha kubaini ufanisi, changamoto pamoja na kutoa mapendekezo kuhusu mwelekeo bora wa kutekeleza mtaala wa ngazi husika.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali za mtihani wa Maarifa ya Jamii ulikuwa mzuri.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani laTanzania kuwa, uchambuzi uliobainishwa kwenye taarifa hii utasaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Jiografia na Historia hivyo, kuinua ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo. Uchambuzi huu utasaidia wakufunzi na walimu tarajali kufanyia kazi dosari zilizobainika na kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji bora na hivyo, kuwa na walimu bora wa somo la Maarifa ya Jamii katika shule za Msingi nchini Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika uandaaji wa taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa.

Dkt. Said Ally Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Maarifa ya Jamii gazi ya cheti, Daraja la III A (GATCE) uliofanyika Mei, 2023 uliandaliwa kwa kuzingatia mihtasari ya mwaka 2009 ya masomo ya Jiografia na Historia ngazi ya ualimu wa Elimu ya Msingi.

Mtihani wa Maarifa ya Jamii uligawanyika katika sehemu mbili A na B zenye jumla ya maswali 14. Sehemu A ilikuwa na jumla ya maswali 10 ya majibu mafupi. Kati ya hayo, maswali nane yalipima taaluma na mawili yalipima utaalamu wa ufundishaji. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama nne hivyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 40. Sehemu B ilikuwa na jumla ya maswali manne ya insha ambapo mawili yalipima taaluma na mawili mengine yalipima utaalamu wa ufundishaji. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama 15, hivyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 60.

Kwa madhumuni ya uchambuzi, ufaulu wa watahiniwa umegawanyika katika makundi matatu. Mfiko wa asilimia za ufaulu katika makundi hayo ni 0 – 39, 40 – 69 na 70 – 100 mtawalia. Ufaulu wa watahiniwa umeoneshwa kwa kutumia takwimu na chati ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano ufaulu wa wastani na rangi nyekundu ufaulu hafifu. Sababu za watahiniwa kupata ufaulu hafifu, wastani au mzuri zimebainishwa. Ili kufafanua hoja zilizotolewa kuelezea majibu ya watahiniwa, Sampuli za majibu ya watahiniwa zimetumika kama vielelezo ili kuonesha namna watahiniwa walivyoweza au kushindwa kujibu maswali yaliyochambuliwa.

Uchambuzi kuhusu ufaulu wa jumla katika mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa mzuri, Jumla ya watahiniwa 4,391 walisajiliwa kufanya mtihani huo. Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 4,353 sawa na asilimia 100 walifaulu kwa daraja A, B, C na D. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii umepanda kwa asilimia 0.03 ikilinganishwa na ufaulu wa watahiniwa katika somo hilo mwaka 2022, ambapo asilimia 99.97 ya watahiniwa walifaulu.

# 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI


## 2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi

Katika mtihani wa Maarifa ya Jamii, sehemu A ilikuwa ya maswali mafupi na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii. Hivyo, watahiniwa wote walifanya maswali hayo. Kila swali lilikuwa na uzito wa alama 4. Kwa ajili ya kufanya uchambuzi na tathmini, ufaulu wa watahiniwa katika kila swali uligawanywa katika makundi matatu; ufaulu hafifu, wastani

na mzuri. Mfiko wa alama katika kila kundi ulikuwa 0.0-1.5, 2.0 – 2.5 na 3.0 – 4.0 mtawalia.


### 2.1.1 Swali la 1: Sayari Dunia

Swali la 1 lilitoka katika mada ya *Sayari Dunia*. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi sababu za kutokea kwa Jua la utosi, Kupatwa kwa jua, Usiku na mchana na Mabadiliko ya misimu. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,353 (100%) ambapo watahiniwa 1,381 (31.73%) walikuwa na ufaulu hafifu. Aidha, watahiniwa 1,655 (38.02%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 1,317 (30.25%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa swali la 1.




**Chati Na.1:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 1.*

Uchambuzi wa ufaulu katika swali la 1 unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walikosa maarifa ya kutosha kwenye mada iliyotahiniwa. Pia, baadhi yao hawakubaini matakwa ya swali. Majibu mengi ya watahiniwa katika kategoria hii yalijikita katika kueleza maana za kupatwa kwa jua na mwezi, vyanzo vya majanga, athari za mzunguko wa Dunia kwenye mhimili wake na changamoto zitokanazo na mikondo baridi ya bahari. Kielelezo Na.1.1 ni Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 1.


1

i/ Jua la utosi : Kutokana kupatwa kwa jua ambapo hutokea dunia, jua na mwezi kuwa katika mstari mmojo

ii/ Kupatwa kwa Jua : ni kitendo cha dunia kuwa katikati ya jua na mwezi hivyo mionzi za Jua hufika majo kwa maja katika dunia

iii/ mabadiliko ya misimu hutokana na kubadilika kwa kwa tabia za nchi ambayo hutokana na majanga ya asili na shughuli za kibinadamu. mfano kiangazi, masika, na vuli:

iv/ Kutokea kwa usiku na mchana: hutokana na mizunguko ya dunia mfano dunia kulizunguka jua.


**Kielelezo Na. 1.1:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 1*

Kielelezo Na.1.1 ni majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmojawapo wa watahiniwa. Kwa mfano, katika kipengele cha (i) mtahiniwa alieleza kimakosa chanzo cha jua la utosi. Mtahiniwa alipaswa kufahamu kuwa jua la utosi hutokana na kitendo cha dunia kuzunguka jua ambapo mkao tenge wa dunia wa nyuzi 23.5 hufanya maeneo mbalimbali ya dunia kupata jua la utosi katika muda/vipindi vinavyotofautiana.

Aidha, uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kwamba watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walitoa hoja ambazo maelezo yake yalikuwa hayajitoshelezi. Aidha, baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo kuwa na ufaulu wa wastani. Vilevile baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walijikita katika kueleza maana ya hali ya hewa na sababu za kutokea kwa jua la utosi au kupatwa kwa jua.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliofanya vizuri walieleza kwa usahihi sababu za matukio hayo ya kijiografia kulingana na matakwa ya swali. Watahiniwa waliofanya vizuri walieleza kuwa, usiku na mchana hutokana na dunia kujizungusha kwenye mhimili wake na Jua la utosi hutokana na dunia kuzunguka jua. Aidha walieleza kuwa kupatwa kwa jua ni tukio linalotokea wakati mwezi unapokuwa katikati ya jua na

dunia. Kwa upande mwingine watahiniwa hao walieleza kuwa jua la utosi ni matokeo ya dunia kuzunguka jua ambapo huwa ni tarehe 21 Machi na 23 Septemba katika Ikweta wakati katika Tropiki ya Kansa ni 21 Juni na katika Tropiki ya Kaprikoni tarehe 22 Disemba. Kielelezo Na.1.2 ni Sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la 1.



1

i) Jua la Utosi
Jua la Utosi husababishwa na dunia kulizunguka jua ambapo hutokea mara nne kwa mwaka yaani Machi 21, Juni 21, Septemba 23 na Disemba 22.
ii) Kupatwa kwa jua.
Kupatwa kwa jua husababishwa na ~~dunia~~ ~~kupita~~ mwezi kupita katikati ya dunia na jua.
iii) Mabadiliko ya Misimu.
Mabadiliko ya misimu husababishwa na dunia kulizunguka jua. ambapo tunapata misimu minne ya kiangazi, Masika, Vuli na kipupwe.
iv) Kutokea kwa Usiku na mchana.
Usiku na mchana hutokea baada ya dunia kujizungusha kwenye mhimili wake.


**Kielelezo Na.1.2:** Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa kwa swali la 1

Katika kielelezo Na.1.2 mtahiniwa alieleza kwa usahihi sababu za kutokea kwa matukio mbalimbali ya kijiografia jambo linalodhihirisha kuwa mtahiniwa alikuwa na uelewa wa kutosha kwenye mada na dhana zilizotahiniwa.

### 2.1.2 Swali la 2: Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani


Swali la 2 lilitoka katika mada ya *Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani*. Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa aeleze umuhimu wa kipimo cha ramani, kichwa cha ramani, dira na ufunguo wa ramani. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,353 ambao ni sawa na (100%). Takwimu zinaonesha watahiniwa 4150 (74.57%) walikuwa na ufaulu mzuri, watahiniwa 142 (22.54%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 61 (2.9%) walikuwa na ufaulu hafifu. Muhtasari wa

kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na.2.




**Chati Na.2:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 2.*

Uchambuzi wa ufaulu katika swali la 2 unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana iliyoulizwa na pia walishindwa kubaini matakwa ya swali. Majibu ya watahiniwa katika kategoria hii yalijikita katika kueleza tofauti ya ramani na picha, aina za vipimo vya ramani na aina za ramani. Kielelezo 2.1 kinaonesha majibu yasiyo sahihi ya swali la 2.



2
i) Husaidia katika Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Vitendo
ii) Hurahisisha mwalimu katika Ufundishaji wake
iii) Kujua na Kutambua mipaka ya nchi
iv) Kutambua au Kurahisisha kazi za kijeshi.

**Kielelezo Na.2.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 2

Majibu ya mtahiniwa katika kielelezo Na. 2.1 si sahihi kwa sababu alieleza jinsi kipimo cha ramani kinavyosaidia katika ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo badala ya kueleza umuhimu wa kipimo cha ramani.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikosa baadhi ya vipengele vya swali husika lakini pia kutoa maelezo yasiyojitosheleza kwenye baadhi ya hoja.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kwamba, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walieleza kwa usahihi umuhimu wa vipengele vya ramani jambo linaloashiria kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani. Kielelezo Na.2.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya swali la 2


2 i) Kipimo husadia kuonesha uwiano kati ya umbali katika ramani na umbali katika ardhi.

ii) Kichwa cha ramani, husaidia kutoa maelekezo kuhusiana na ramani inachokiwakilisha katika mazingira halisi.

iii) Dira, husaidia kuonesha muelekeo wa pande kuu za dunia katika ramani.


iv) Ufunguo; husaidia kuonesha alama mbalimbali zilizotumika katika ramani zinawakilisha uhalisia wa kitu gani. Mfano: ■ kuwakilisha mji mkuu.

**Kielelezo Na.2.2:** Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali la 2

Katika kielelezo Na.2.2 mtahiniwa alieleza na kuthibitisha kwa usahihi umuhimu wa dira, kichwa cha ramani, kipimo na ufunguo katika ramani.


### 2.1.3 Swali la 3: Sayari Dunia

Swali la tatu (3) limetoka kwenye mada ya *Sayari Dunia.* Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa abainishe kwa ufupi mambo manne yanayoweza kusababisha majanga ya asili. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,353 (100%) ambapo watahiniwa 2,730 (63%) walikuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa 1,468 (34%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 155 (3%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na.3:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 3.*

Uchambuzi wa ufaulu katika swali la 3 unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hili walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya matakwa ya swali kuhusu mada ya Sayari Dunia hivyo, walibainisha kwa usahihi sababu za kutokea kwa majanga ya asili kama vile *milipuko ya ardhi, mvua kubwa, upepo mkali, milipuko ya volcano*. Kielelezo Na.3.1 ni Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 3.


3 (a) Tetemeko la ardhi: ambalo husababishwa na Mvutano wa kani.
(b) Ukame: huweza kusababishwa kutokana na Ongezeko la joto duniani.
(c) Mafuriko husababishwa na kunyesha kwa mvua nyingi kupita kiasi na mito kuweza kujaa na kusambaza maji hadi sehemu za makazi ya watu.
(d) Mlipuko wa Volkano: husababishwa na kutokea kwa mgandamizo wa kani ambapo husababisha Magma kutokea juu ya ardhi.

**Kielelezo Na.3.1:** Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa.

Katika kielelezo Na.3.1, mtahiniwa alibainisha na kueleza kwa usahihi matukio yanayoweza kusababisha majanga ya asili.

Uchambuzi unaonehsa kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani waliandika hoja zilizo sahihi lakini zisizo na maelezo au ufafanuzi wowote.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kubainisha na kueleza kwa usahihi mambo yanayoweza kusababisha majanga ya asili. Watahiniwa katika kategoria hii walikosa maarifa ya kutosha kuhusu majanga ya asili kwa mfano, baadhi ya majibu ya watahiniwa yalihusu *ufugaji mifugo, ujenzi wa maeneo yenye miteremko, ukataji wa miti, kuongezeka kwa watu, maendeleo ya sayansi na teknolojia na watu kujenga karibu na mabonde* na yalijikita katika kuelezea sababu zisizo za asili za kutokea kwa majanga. Kielelezo Na.3.2 ni Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

3

i) Uchafuzi wa Mazingira

ii) Ukataji wa miti ovyo

iii) Ufugaji wa Mifugo Mingi katika eneo dogo.


iv) Ukosefu wa Elimu juu ya Utunzaji wa Mazingira

**Kielelezo Na.3.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi. katika swali la 3.

Majibu ya mtahiniwa katika kielelezo Na. 3.2 yanadhihirisha kuwa hakuelewa matakwa ya swali. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa abainishe kwa ufupi mambo manne yanayoweza kusababisha majanga ya asili lakini mtahiniwa alieleza namna majanga yanavyotokea kutokana na shughuli za kibinadamu.

### 2.1.4 Swali la 4: Nchi yetu Tanzania

Swali la nne (4) lilitoka katika mada ya *Nchi yetu Tanzania*. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma takwimu za tabia nchi kutoka kwenye jedwali alilopewa na kisha kubaini miezi yenye hali ya hewa ya baridi, kukokotoa wastani wa kiwango cha mvua kwa mwezi, kubaini aina ya tabia nchi ya eneo husika na sababu zake, kubaini miezi yenye kiwango cha juu cha joto. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,343 (100%) ampapo watahiniwa 2,336 (53.64%) walikuwa na ufaulu hafifu. Aidha watahiniwa 1,207 (27%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 810 (18.61%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na.4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4.




**Chati Na.4:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 4.*

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4 unaonesha waliokuwa na ufaulu wa juu. walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Nchi yetu Tanzania kwani waliweza kutoa majibu sahihi kulingana na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 4.1 ni Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali la 4.

4 i) Mwezi, Januari, februari, machi, april, mei, Julai Agosti, septemba, oktoba, novemba, na desemba - kwa sababu jotoridi la°C ni 27° inapidi liwepo.

ii) = Wastani = jumla / Idadi.

= 50.8 + 38.1 + 33.0 + 20.3 + 20.3 + 17.8 + 7.6 + 10.2 + 15.2 + 48.2 + 73.7 + 61 / 12 = 391.2 = 32.6

= Wastani = 32.6.

iii) i) Tabia ya kimedtrenia. kwa sababu jotoridi ni 32°C (ii) mvua huwa hunyesha kwa kiangazi.

iv) Miezi julai na juni. - kwa sababu Jotoridi ni chini ya 27 °C


ii) Mvua huwa ni ya kiangazi. Wingi sana.

**Kielelezo.Na.4.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 4.

Katika kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alibaini hali ya hewa, tabia ya nchi na kutumia kanuni sahihi kukokotoa wastani wa kiwango cha mvua kwa mwezi.

Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walitoa jibu sahihi kwenye kipengele kimoja au viwili kati ya vipengele vinne vya swali. Mfano, watahiniwa wengi waliokuwa na ufaulu wa wastani walikosa kipengele cha (ii) na kipengele cha (iii) kwa sababu walishindwa kuainisha kanuni ya kutafuta wastani wa mvua kwa mwezi na hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Tabia Nchi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walitoa majibu yasiyo sahihi kulingana na matakwa ya swali. Majibu yasiyo sahihi yametokana na kushindwa kusoma na kutafsiri vema data za Tabia ya Nchi zilizokuwa katika jedwali pamoja na kushindwa kufanya hesabu za kukokotoa wastani wa mvua na kupendekeza aina ya tabia ya nchi. Kielelezo Na. 4.2 kinaonsha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 4



4 (i) J Mvua 7.6, Kwasababu kuna baridi kali ninge mshauri aende na nguo za kujikinga na baridi.
(ii) Wastani wa milimeta 20.3.
(iii) aina mbili kwa sababu, mvua hunyesha mala moja kwa mwaka,
(iv) J 26.6°C Joto, kwa sababu kuna joto kali namshauri avae nguo za kawaida

**Kielelezo Na. 4 .2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi la swali la 4.

Majibu ya mtahiniwa katika kielelezo Na. 4.2 sio sahihi kwa sababu hakuweza kukokotoa kwa usahihi na kubainisha aina ya Tabia Nchi kwenye mji husika. Pia, alishindwa kubainisha miezi yenye baridi na aina gani za nguo ili kujikinga na baridi.


### 2.1.5 Swali la 5: Maandalizi ya kufundisha na kujifunza

Swali la tano (5) lilitoka katika mada ya *Maandalizi ya kufundisha na kujifunza* ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi namna mwalimu anavyoweza kutumia azimio la kazi, andalio la somo, shajara ya somo pamoja na nukuu za somo katika ufundishaji wa somo la Jiografia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,353 (100%) ambapo watahiniwa 455 (10.45%) walikuwa na ufaulu hafifu. Aidha, watahiniwa 1,113 (25.57%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 2,785 (63.98%) walikuwa na ufaulu mzuri, kama Chati Na. 5. Inavyoonesha.




**Chati Na.5:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 5.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walieleza kwa usahihi namna azimio la kazi, andalio la somo, shajara na nukuu za somo zinavyotumika katika ufundishaji wa somo la Jiografia. Mfano wa majibu ya watahiniwa waliojibu kwa usahihi ni kama vile; *andalio la somo humsaidia mwalimu kufundisha kwa kufuata hatua za somo bila kutoka nje ya mada, sharaja husaidia kuonesha mada na muda zilivyofundishwa na Shajara; hutumika kutunza kumbukumbu za ufundishaji, hutumika kuonesha mada zilizofundishwa na muda uliotumika kufundisha pia hutumika kupima kasi ya ufundishaji wa somo la Historia*. Kielelezo Na. 5.1 ni Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali la 5



5 i) Azimo la kazi hutumika kwa kuonyesha mada zote zinazotarajiwa kufundishwa kutoka kwenye muhtasari, hivyo humwongoza mwalimu kile kinacho takiwa kufundishwa.
ii) Andalio la somo, hutumika kwa kuongoza mwalimu katika ufundishaji wake kwa namna tofautitofauti kama vile kufundisha kwa hatua, matumizi ya zana na kutathimini somo.
iii) Shajara hutumika kwa kuonyesha taarifa za mada zilizofundishwa na muda uliotumika kufundisha mada hizo,
iv) Nukuu za somo, hutumika kwa kusoma maarifa ya mada inayotarajiwa kufundishwa, hii husaidia kwa mwalimu kutayarisha maarifa kwa kuyanakili yanayopaswa kufundishwa.

**Kielelezo 5.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5.

Katika kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa alieleza kwa ufasaha namna anavyoweza kutumia azimio la kazi, andalio la somo, shajara na nukuu za somo katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kueleza namna mwalimu anavyoweza kutumia nyaraka hizo katika kufundisha somo la Jiografia hivyo kuwa na ufaulu wa wastani.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walichanganya hoja za umuhimu wa nyaraka za kufundishia somo la Jiografia hususani umuhimu wa andalio la somo na umuhimu wa azimio la kazi. Pia, baadhi ya watahiniwa walishindwa kutofautisha kati ya umuhimu wa nyaraka hizo na maana ya nyaraka hizo. Aidha, wapo watahiniwa waliotoa hoja chache tofauti na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.


5

i) kumrahisisha mwalimu katika ufundishaji wa somo lake

ii) Humfanya mwalimu kujiami wakati anapo fundisha

iii) Humsaidia mwalimu kutumia njia na mbinu bora za kufundisha na kujifunzia


iv) Humsaidia mwalimu kufikia malengo mahususi ya somo

**Kielelezo Na.5.2** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.

Katika kielelezo Na.5.2, mtahiniwa, badala ya kuelezea namna atakavyo tumia nyaraka za kufundishia ambazo ni azimio la kazi, andalio la somo, shajara na nukuu za somo, alieleza umuhimu wa andalio la somo.


### 2.1.6 Swali la 6: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika

Swali la 6 lilitungwa kutoka katika mada ya *Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika.* Swali lilimtaka mtahiniwa kukanusha kauli kuwa kutawaliwa kwa bara la Afrika na mataifa ya Ulaya kulitokana na udadisi na ugunduzi wa kisayansi na siyo malengo ya kiuchumi. Hivyo, mtahiniwa alipaswa kueleza sababu za kiuchumi za kutawaliwa kwa bara la Afrika. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,353 (100%) ambapo watahiniwa 724 (16.6%) walikuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa 1,289 (29.6%) ufaulu wa wastani na watahiniwa 2,340 sawa na asilimia 53.8 walikuwa na mzuri hafifu. Chati Na.6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6.




**Chati Na.6:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 6.*

Uchambuzi wa ufaulu katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufauluk mzuri walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika na walielewa vizuri matakwa ya swali hivyo, kutoa majibu sahihi. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya jibu la mmoja wa watahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



6 i) Kupata sehemu za uwekezaji, wakoloni walikuja bara la Afrika kwa lengo la kupata sehemu za uwekezaji kwa ajili ya biashara zao na pia uendelezaji wa kisayansi.
ii) malighafi, pia wakoloni waligawanya na kutawala Afrika kwa sababu ya kupata malighafi zitakazo wasaidia huko kwenye uchumi wao na pia uendelezaji wa kisayansi.
iii) kutafuta sehemu zenye madini, wakoloni walitawala Afrika kwa sababu walikua wakitafuta sehemu zenye madini kwa ajili ya uchumi na pia uendelezaji wa kisayansi
iv) kutafuta masoko, walitawala Afrika ili waweze kupata masoko watakayo uza bidhaa zao ili waweze kuinua uchumi na kukuza maendeleo nchini kwao na pia uchunguzi wa kisayansi.

**Kielelezo Na.6.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6

Katika kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alieleza kwa ufasaha sababu za kiuchumi zilizosababisha mataifa ya Afrika kutawaliwa na Nchi za Ulaya.

Aidha watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani waliorodhesha hoja bila kutoa maelezo. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi hivyo kupata ufaulu wa wastani. Hii ilisababishwa na watahiniwa hawa kutofuata maelekezo ya swali kwani baadhi yao walitoa tu sababu bila kutoa maelezo mafupi na wengine walitoa majibu yasiyoendana na matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu. walichanganya dhana ya sababu za kutawaliwa kwa bara la Afrika na dhana nyinginezo kama vile mbinu/njia zilizotumika katika kuimarisha utawala wa kikoloni kama vile mikataba ya ulaghai na kujenga ngome za kiutawala na kijeshi. Mtahiniwa alichanganya matakwa ya swali. Kielelezo Na 6.2 ni mfano wa majibu yasiyo sahihi ya swali la 6


6
i) Kuunda mifumo mbalimbali ya kutawala - mfumo wa mlango wa nyuma, mfumo
Kasumba, mfumo wa mlango wa nyuma.
ii) Kuunda ngome za kiutawala na kijeshi ili kukabiliana na upinzani
iii) Kujenga miundombinu mbalimbali kama shule ambapo ilisaidia kuimarisha utawala
iv) ... au kushawishi watawala na kuingia mikataba ya ... ya utawala ...


**Kielelezo Na.6.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 6

Katika Kielelezo Na.6.2, mtahiniwa alieleza namna watawala wa kikoloni walivyoweza kuimarisha utawala wao katika makoloni yao kwa mfano, kujenga miundombinu kama shule, kuunda mifumo mbalimbali ya kiutawala kama vile muundo wa mlango wa nyuma,

kuwahusisha watawala wa kijadi badala ya kueleza sababu za kiuchumi zilizofanya mataifa ya Ulaya kutawala Bara la Afrika.

### 2.1.7 Swali la 7: Ufundishaji wa Mada za Somo la Historia

Swali la 7 lilitoka katika mada ya *Ufundishaji wa Mada za Somo la Historia.* Swali lilimtaka Mwalimu wa somo la Historia kuwafundisha wanafunzi mada ya Vitangulizi vya Ukoloni. Watahiniwa 4,353 (100%) walifanya swali hilo ambapo watahiniwa 126 (2.89%) walikuwa na ufaulu hafifu. Aidha watahiniwa 981 (22.54%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 3,246 (74.57%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7.




**Chati Na.7:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 7.*

Uchambuzi wa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuriulikonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Ufundishaji wa mada za somo la Historia* hivyo, walieleza kwa usahihi mbinu zinazoweza kutumika kufundishia mada husikakama vile: Usomaji bainifu wa maandishi matumizi ya picha na ramani, hadithi na kujifunza kwa ziara. Kielelezo Na 7.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya swali la 7.

7 i) Kualika mgeni, mbinu hii anaweza kuitumia mwalimu kwa kumualika mtaalamu wa mada hiyo ili aweze kuielezea kwakina

ii) Maswali na majibu, katika mbinu hii mwalimu atakuwa anawauliza wanafunzi wake maswali na kisha wao kujibu

iii) Mbinu ya majadiliano, mwalimu atawaruhusu wanafunzi waweze kujadiliana kuhusu kile wanachokijua kutokana na mada husika


iv) Ziara mafunzo, katika mbinu hii mwalimu atawapeleka wanafunzi sehemu mbalimbali ambazo vitangulizi vya ukoloni vilifikia

**Kielelezo Na.7.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 7.

Katika kielelezo Na.7.1 mtahiniwa alielewa matakwa ya swali na pia alikuwa na umahiri kuhusu mbinu nne anazoweza kutumia mwalimu wa somo la Historia kuwafundisha wanafunzi mada ya Vitangulizi vya Ukoloni.

Aidha watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastaniwalitoa hoja bila maelezo ya kutosha au kutoa hoja chache tofauti na matakwa ya swali.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha kwenye mada iliyotahiniwa. Aidha, baadhi yao walishindwa kuelezea athari za *Vitangulizi vya Ukoloni*. Hata hivyo, watahiniwa wengine waliweza kuelezea hoja moja sahihi kati ya nne. Halikadhalika, watahiniwa wengine walieleza hoja chache tofauti na matakwa ya swali. Kielelezo Na.7.2 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 7.




7 Mbinu za kuwafundishia wanafunzi mada ya vitangulizi vya ukoloni, Mbinu hizo ni
(i) Kutumika kwa mbinu ya mahojiano ambayo ilitumiwa na wapelelezi kupeleleza maisha ya waafrika ili kujeng-a mahusiano mema.
(ii) Wamisionari ambao walikuja Afrika kwa lengo la kueneza dini ya kikristo mfano kujenga makanisa kama vile (M.C.M) Missionary centre.
(iii) Wafanyabiashara ambao lengo ilikuwa ni kujua hali ya kiuchumi ya waafrika ili kupata nafasi ya kuweka bidhaa.
(v) Walitumia mbinu ya udadisi, ili kupata maliasili walizonazo waafrika kama vile vyanzo vyenye madini, misitu.

**Kielelezo Na.7.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 7

Katika Kielelezo Na.7.2. mtahiniwa alieleza mbinu walizo tumia wakoloni ili kupata maeneo ya uwekezaji, kupata malighafi na kupata masoko, badala ya kuelezea mbinu ambazo anaweza kutumia mwalimu wa somo la Historia kuwafundisha wanafunzi mada ya Vitangulizi vya Ukoloni.


### 2.1.8 Swali la 8: Mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika huru

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika huru.* Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi hoja nne za kupinga mtazamo kwamba hakuna hatua zozote zilizopigwa na nchi za Kiafrika tangu zilipojipatia uhuru kutoka kwa wakoloni. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,343 (100%). Kati yao, watahiniwa 1,365 (31.4%) walikuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa 1,378 (31.7%) ufaulu wa wastani na watahiniwa 1,610 (37.0%) ufaulu mzuri kama inavyooneshwa katika Chati Na.8




**Chati Na.8:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 8.*

Uchambuzi wa ufaulu unaonesha kuwa watahiniwa 1, waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika huru.* Hii iliwawezesha kuelewa kwa ufasaha mahitaji ya swali hivyo, walieleza kwa usahihi hatua zilizopiga nchi nyingi za Kiafrika tangu kujipatia uhuru kama vile, maendeleo ya viwanda, maendeleo ya miundombinu, kutatua migogoro mbalimbali na maendeleo ya kilimo. kielelezo Na. 8.1 ni Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 8.



8 Hatua zilizopigwa na nchi za kiafrika tangu kujipatia uhuru.
(i) Maendelo ya viwanda katika uzalishaji wa bidhaa.
(ii) Maendelo katika kuboresha miundombinu kama vile barabara na reli
(iii) Ukuaji katika mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano kama vile simu, kompyute na ndege.
(iv) Maendeleo katika utolewaji wa huduma za Elimu na matibabu kwa nchi za Afrika.

**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 8

Katika kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa alieleza hatua nne ambazo nchi za Afrika zimepiga tangu kujipatia uhuru wake kutoka kwa wakoloni.

Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani baadhi yao walitoa hoja pungufu, na wengine walishindwa kutoa sababu zilizojitosheleza. Aidha, watahiniwa wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika majibu yao. Lakini pia, wapo baadhi ya walioorodhesha hoja pasipo kutoa maelezo yoyote. Kwa ujumla, hoja zilizotolewa na watahiniwa wengi katika kundi hili zinaashiria kuwa baadhi ya watahiniwa walikuwa na maarifa ya wastani katika mada ya Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika huru.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walikosa maarifa ya kutosha kwenye mada iliyotahiniwa. Pia, baadhi ya watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja hakuelewa kiini cha swali hivyo, kutoa hoja ambazo hazipingi hoja bali akakubaliana na hoja kuwa tangu nchi za Afrika kupata uhuru hakuna hatua walizopiga, alieleza hoja kama vile, *uchumi mbovu, miundombinu ya barabara mibovu, huduma za jamiii kama vile maji, shule na afya ni mibovu*. Aidha mtahiniwa mwingine alieleza hoja zisizo sahihi kama vile, *kutokuwepo kwa ushirikiano, ulipaji mkubwa wa kodi, uhaba wa ajira na uhaba wa miundombinu*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile, *mtazamo wa kielimu, mtazamo wa kidini, mtazamo wa kisiasa na mtazamo wa kiutamaduni*. Kwa ujumla watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha na hawakuelewa nini swali linataka. Kielelezo Na. 8.2 ni Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.



8
i) Njia ya vita
ii) Njia ya amani
iii) Njia ya ~~mapinduzi~~ Mapinduzi
iv) Njia ya Maelewano.

**Kielelezo Na. 8.2:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.*

Katika Kielelezo Na.8.2, mtahiniwa alielezea njia zilizotumika kudai na kupigania Uhuru Barani Afrika badala ya kueleza hatua zilizopiga nchi za Kiafrika tangu kupata Uhuru.


### 2.1.9 Swali la 9: Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika

Swali la 9 lilitoka katika mada ya *Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika*. Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze kwa ufupi sababu nne za kushindwa kwa jamii nyingi za Kiafrika katika mapambano yao dhidi ya uvamizi wa Kikoloni. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,343 (100%). Kati yao watahiniwa 208 (4.8%) walikuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa 858 (19.7%) ufaulu wa wastani na watahiniwa 3287 (75.5%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na.9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa swali la 9.




**Chati Na.9:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 9.*

Uchambuzi wa ufaulu ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika.* Hivyo, walitaja kwa usahihi sababu za jamii nyingi za kiafrika kushindwa katika mapambano yao dhidi ya wakoloni. Kwa mfano, *kukosa ushirikiano, usaliti kwa baadhi ya viongozi na zana duni za kivita.* Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya swali la 9.


9 (i) Kwa sababu walikosa ushirikiano na umoja, jamii nyingi zilikuwa na usaliti kiasi kwamba kwa walipelekea hadi kushindwa.
(ii) Kwa sababu walikuwa na silaha duni, hii pia ni sababu nyingi kwamba walipigwa walishindwa kwa sababu walikuwa na silaha duni.
(iii) Kwa sababu hawakuwa na uongozi imara na majeshi ya kutosha, pia hii sababu nyingine kwamba walipigwa hawakuwa na uongozi imara.
(iv) pia ni usaliti miongoni miongoni mwa baadhi ya viongozi waliokuwa wasaliti hadi ilipelekea hadi kushindwa kitu au mapambano dhidi ya ukoloni.


**Kielelezo Na.9.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 9.

Katika kielelelezo Na.9.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi sababu zilizofanya jamiii nyingi za Kiafrika kushindwa katika mapambano yao dhidi ya wakoloni.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada husika hivyo, wengi wao waliorodhesha sababu chache bila maelezo yoyote tofauti na matakwa ya swali na baadhi yao walirudia hoja walizokuwa wamezieleza

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuwa na maarifa juu ya mada iliyopimwa hivyo, walitoa hoja pungufu, na wengine waliandika majibu ambayo ni shughuli mbalimbali walizokuwa wanafanya wavumbuzi, wamisionari na wafanyabiashara ili kukamilisha malengo yao ya kuja Afrika. Kwa mfano; *Kuanzishwa kwa biashara ya utumwa, kuanzishwa kwa kilimo cha mazao ya biashara, kuanzishwa kwa dini mbalimbali, kuanzishwa kwa viwanda mbalimbali*. Aidha, mtahiniwa mwingine badala ya kuandika sababu zilizosababisha jamii nyingi za kiafrika kushindwa katika mapambano yao dhidi ya wakoloni, alitoa majibu yaliyowafanya wakoloni kuja Afrika. Majibu aliyotoa ni kama vile,

*walikuja kutafuta maeneo ya kuanzisha biashara, walikuja kutafuta malighafi, kutafuta maeneo yenye rutuba, walikuja kutafuta wafanyakazi*. Majibu ya namna hii yanaashiria kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa mahususi kuhusu sababu za jamii nyingi za kiafrika kushindwa katika mapambano yao dhidi ya wakoloni. Vilevile, baadhi ya watahiniwa katika kundi hili hawakuandika chochote, na wengine waliandika majibu ambayo yaliashiria hawakuelewa matakwa ya swali. Hivyo, walitoa majibu ambayo hayakuendana na swali. Kielelezo Na. 9.2 ni Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 9.


9

i) Uharibifu wa miundo mbinu mbalimbali mfano - Reli na Barabara
ii) Vifo; Ilitokea kwa waafrika na wazungu, takini - waafrika wengi waliuawa kwa sababu silaha zao zilikuwa - duni.
iii) Kushuka kwa shughuli za kiuchumi; Kutokana na ukosefu wa uhirikiano baina ya wazungu na waafrika.
iv) Njaa kutokana na kutokuzalisha
v) Kubadilika kwa njia ya kiuongozi; Wazungu walikuwa wanawalazimisha waafrika kufanya kazi katika mashamba na kulipwa mshahara mdogo.


**Kielelezo Na. 9.2**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 9.

Katika kielelezo Na.9.2, mtahiniwa alieleza athari za vita badala ya kuelezea sababu za jamii nyingi za kiafrika kushindwa katika mapambano yao dhidi ya wakoloni.

### 2.1.10 Swali la 10: Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru

Swali la 10 lilitoka katika mada ya *Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika huru*. Swali lilimtaka mtahiniwa atumie hoja nne kueleza kwa ufupi changamoto ambazo nchi za kiafrika zilikumbana nazo mara baada ya kupata uhuru. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,343 (100%) ambapo watahiniwa 1,072 (24.6%)

walikuwa na ufaulu hafifu. Vilevile watahiniwa 1,031 (23.7%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 2,250 (51.7%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na.10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa swali la 10.




**Chati Na.10:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 10.*

Uchambuzi wa ufaulu katika swali hilo unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika huru hivyo, walieleza vizuri changamoto zilizozikumba nchi nyingi za Kiafrika baada ya Uhuru kama vile, *njaa, uhaba wa nguvu kazi na ukosefu wa wataalamu katika fani mbalimbali.* Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.

| | |
|---|---|
| 10 | i/ Uhaba wa huduma za Afya kutokana na upungufu |
| | wa hospitali, zahanati madawa na wataalamu, kwa |
| | mfano wauguzi na madaktari. |
| | |
| | ii/ Miundombinu mibovu kwa mfano kulikuwa na |
| | majengo yaliyochakaa ya madarasa, barabara mbovu |
| | na zilizoharibika |
| | |
| | iii/ Upungufu wa wataalamu wenye elimu kama vile |
| | wakandarasi, madaktari, walimu na wanasheria. |
| | |
| | iv/ Waafrika wengi walikuwa masikini na |
| | hawakuwa na ajira wala shughuli za kufanya |
| | kwa lengo la kuingiza kipato |


**Kielelezo Na.10.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 10.

Katika kielelezo Na,10.1, mtahiniwa alikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu changamoto ambazo nchi za Kiafrika walikumbana nazo baada ya Uhuru na alielewa matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani waliorodhesha sababu chache ambazo hazikufika nne (4) kama swali linavyotaka wakati hoja nyingine hazikuelezewa kwa usahihi hivyo, kufanya kupata ufaulu wa wastani.

Pia, uchambuzi wa ufaulu katika swali la 10 unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walikosa maarifa ya kutosha juu ya mada iliyotahiniwa hivyo, walieleza athari za ukoloni badala ya kueleza changamoto ambazo mataifa ya Kiafrika yalikabiliana nazo baada ya kupata Uhuru. Mifano ya majibu yasiyo sahihi ya watahiniwa ni kama vile; *kulikuwa na biashara ya utumwa, kulikuwa na kodi za vichwa, kuvurugika kwa familia za kiafrika, waafrika wengi walikufa, kulikuwa na ubaguzi wa rangi*. Aidha, mtahiniwa mwingine alijikita katika kuelezea mafanikio baada ya uhuru badala ya changamoto. Alieleza hoja kama vile *maendeleo ya viwanda, ubora wa miundombinu, watu kuongezeka*, mtahiniwa mwingine aliezea hoja kama vile, *kutofautiana kwa lugha, tofauti za kiitikadi, kutofautiana kwa thamani ya fedha na kutofautiana kwa maendeleo ya sayansi na*

*teknoloji*. Majibu kama hayo yanaashiria watahiniwa hawakuwa na umahiri wa kutosha katika mada ya Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika huru. Kielelezo Na. 10.2 ni Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 10.


10

i) Kutawanyika kwa familia nyingi za Waafrika.

ii) Kuharibiwa kwa sekta za uzalishaji mali mfano katika kilimo. Ona mazao.

iii) Waafrika wengi walikufa - Walikufa kutokana na mateso makali.

iv) Kuchukuliwa kwa malighafi mfano madini, dhahabu na almasi na wakoloni.

**Kielelezo Na.10.2**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 10


Katika kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa alieleza athari za ukoloni barani Afrika badala ya kuelezea changamoto zilizozikumba nchi za Kiafrika baada ya kupata uhuru.

## 2.2 Sehemu B: Maswali ya Insha

Sehemu B katika mtihani wa Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali manne ya insha ambayo mtahiniwa alitakiwa kuyajibu yote. Maswali mawili ya taaluma; moja lilihusu somo la Jiografia na moja somo la Historia. Pia, kulikuwa na maswali mawili ya ufundishaji na ujifunzaji; moja lilihusu somo la Jiografia na moja somo la Historia. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na uzito wa alama 15. Kwa ajili ya kufanya uchambuzi na tathmini, ufaulu wa watahiniwa katika kila swali uligawanywa katika makundi matatu; ufaulu hafifu, ufaulu wa wastani na ufaulu mzuri. Mfiko wa alama katika kila kundi ulikuwa 0-5.5, 6-10.0 na 10.5-15 mtawalia.

### 2.2.1 Swali la 11: Sayari Dunia

Swali la 11 lilitoka katika mada ya *Sayari Dunia.* Swali lilimtaka mtahiniwa atumie hoja tano kufafanua umuhimu wa nguvu za jua katika maisha ya binadamu katika Sayari Dunia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,343 (100%) ambapo watahiniwa wanne (4) (0.1%) walikuwa na ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 138 (3.2%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 4,211 (96.6%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na.11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa swali la 11.




**Chati Na.11:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 11.*

Kulingana na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Sayari Dunia*, walielewa matakwa ya swali hivyo walitoa majibu sahihi. Kielelezo Na.11.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya ya mmoja wa watahiniwa.

11

Jua: Ni gimba Lenye nuru kali lililopo angani ambalo hutoa mwanga na joto na lipo katikati ya Sayari zote. katika mfumo wa jua zipo sayari ambazo ni kubwa kuliko nyingine na zipo Sayari ambazo ni ndogo kuliko nyingine. Sayari ambayo ni kubwa huitwa Sumbula na sayari ambayo ina pete huitwa Zarafeini na ambayo ipo mbali na jua ni Zohari.

Sayari Dunia ni sayari pekee ambayo huishi Viumbe hai mfano wanyama miti binadamu - kwa sababu sayari dunia kuna uwepo wa vitu mbalimbali kwa ajili ya maisha ya binadamu mfano maji, hewa ya oksijeni, wanyama, chakula

Ufuatao ni Umuhimu wa Jua katika maisha ya binadamu katika sayari dunia.

Jua hutupatia Vitamini "D" wakati jua linapochomoza huweza kuwapatia Viumbe hai Vitamini wakati wanapokuwa wanaota jua na wakati jua linapozama pia huweza kuwapatia Viumbe hai Vitamini Uthibitisho huu Ulithibitishwa na wanasayansi hivyo basi jua huweza kutupatia Vitamini wakati wa asubuhi wakati linapochomoza na wakati linapo zama wakati wa jioni.

Jua hutusaidia kukaushia Vitu mbali mbali mfano Mazao, nguo. jua hutusaidia katika Ukaushaji wa mazao wakati ya kiwa shambani au yakiwa nyumbani mfano mahindi, pia huweza kutusaidia kukaushia nguo ambazo zimefuliwa ili zikauke na zitumike tena.

**11 Cont.**

Jua husaidia mimea kujitengenezea chakula chake mwenyewe (usanisi nuru) jua husaidia mimea kupata chakula kwa sababu ya uwepo wa jua husaidia katika ukuaji wa mimea jua husaidia pia katika kustawisha mimea kwa sababu mmea unajitengenezea chakula chake mwenyewe hivyo mmea humweza kukua

Jua hutupatia nishati mbalimbali kama nishati ya umeme nishati ya joto jua pekee ndio humweza kutupatia tunaweza kupata mwanga kwa kutumia jua kwa sababu jua ndio tunaweza kutumia katika matumizi ya paneli mbalimbali kama sola ili tuweze kupata mwanga pia jua hutupatia nishati ya joto wakati wa baridi hivyo basi jua ni muhimu katika maisha

Jua hutusaidia katika utengenezaji wa mvua au hutupatia mvua. kwa sababu jua linapopiga kwenye mabonde ya maji, mito, Bahari unyevunyevu hupanda mawinguni ili kutengeneza mawingu mazito kwa ajili ya mvua hivyo basi jua pia humweza kutupatia mvua.

Hivyo basi sayari dunia ni sayari pekee ambayo huishi viumbe hai kwa sababu ya uwepo wa maji, hewa na chakula hivyo basi sayari dunia ndio huwepo na jua ambalo jua ni chanzo pekee cha uwepo wa maisha ya binadamu jua hutumika katika kuzalisha nishati mbalimbali kama nishati ya mwanga, joto na hutupatia vitamini mbalimbali kama vitamini "D" kwenye mwili wa binadamu.

**Kielelezo Na.11.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 11


Katika kielelezo Na.11.1, mtahiniwa alieleza kwa ufasaha umuhimu wa nguvu za jua kwa binadamu katika sayari ya Dunia.

Aidha, uchambuzi wa majibu ulionesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walikuwa na mapungufu katika maelezo yao

kwenye baadhi ya hoja. Lakini pia watahiniwa hao walichanganya hoja sahihih na zisizosahihi. Baadhi ya majibu ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani ni kama vile; *Jua husaidia kupata hewa ya oksijeni, chanzo cha vitamin b, husaidia katika kupikia.* Katika majibu hayo, hoja mbili za mwanzi siyo sahihi ingawa hoja ya mwisho (husaidia katika kupika) ni sahihi kwa kuwa nguvu za jua zinaweza kuvunwa na kuwa umeme ambao unaweza kutumika kupikia. Aidha baadhi ya watahiniwa walishindwa kutoa utangulizi mzuri na hitimisho na kusababisha ufaulu wa wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wanne (4) ambao ni asilimia 0.2 ya waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Sayari Dunia* hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Baadhi yao walichanganya dhana mbalimbali za kijiografia kama vile umuhimu wa jua kuchanganywa na matukio ya usiku na mchana, majira ya mwaka na matukio ya kupatwa kwa jua.

Mifano ya majibu ya watahiniwa waliofanya vibaya ni kama *vile; jua huwezesha kupatikana kwa usiku na mchana, huwezesha kupatikana kwa majira ya mwaka, husaidia miili kupata vitamin B, jua husaidia kupata utofauti wa urefu na mchana* na *husaidia kupatwa kwa jua la utosi.* Kielelezo Na.11.2 ni Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 11.


11

Sayari Dunia; Ni Sayari ya tatu katika Mfumo wa jua; katika Sayari hii ndomo viumbe hai wanopatikana, Sayari dunia Inajizungusha katika mhili wake kwa siku 365¼ au 366. kuna mizunguko miwili ya dunia ambayo ni dunia Kujizungusha yenyewe kwenye mhili wake na Dunia kulizunguka jua. Ufuatao ni umuhimu wa nguvu za jua katika maisha ya binadamu katika Sayari Dunia;

Husababa kupata majira ya mwaka; nguvu za jua kuhusababa kupata majira ya mwaka mfano kiangazi, kipupwe, vuli na masika pale dunia inapozunguka jua ili kukamilisha mzunguko wake ambapo majira haya yanatokea wakati tofautitofauti au miezi tofautitofauti mfano masika mwezi wa kumi nambili pamoja na mwezi wa kwanza hadi wa pili kiangazi konatokea mwezi wa tano hadi mwezi wa tisa kwa baadhi ya maeneo.

Husababa kupatwa kwa jua la utosi; jua la utosi hutokea 21 march na 23 Septemba ambapo jua hili hutokea kutokana na nguvu za jua katika dunia kulizunguka jua, katika mchakato huu jua huwa katika Tropiko ya kansa 21 June na Jua huwa katika Tropiko ya kaprokoni 23 Desemba

Husababa kutokea kwa kupatwa kwa mwezi; hali hii inatokea pale dunia inapokuwa kati ya mwezi na Jua ambapo tukio hili linatokea kutokana na nguvu ya mvutano wa Jua katika mchakato wa dunia kulizunguka jua ambapo kupatwa kwa mwezi kunatokea

11 Cont.

Husaidia kupata utofauti wa usiku na mchana; lakini pia nguvu za jua katika sayari dunia ambapo dunia inapolizunguka jua hali hii inapelekea kuweze kupata utofauti wa usiku na mchana katika vipindi tofautitofauti

Husaidia kutokea kwa kupatwa kwa jua; hali hii hutokea pale mwezi unapokuwa kati ya jua na dunia ambapo inatokana na nguvu za jua katika mchakato wa dunia kulizunguka jua katika mhimili wake

Hata hivyo; Dunia ina mwezi mmoja ambapo husafiri pamoja katika kulizunguka jua na mwezi huakisi mwanga kutoka kwenye jua. Dunia hulizunguka jua na hapohapo mwezi huizunguka sayari dunia na mwezi huviondoa vitu ambavyo vinaielekea sayari dunia ambavyo vingeleta madhara katika sayari hii.


**Kielelezo Na.11.2**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 11.

Katika kielelezo Na.11.2, mtahiniwa alieleza tukio la Kupatwa kwa Jua, Kupatwa kwa Mwezi, Jua la Utosi na Majira ya Mwaka badala ya kueleza umuhimu wa nishati ya jua kwa maisha ya viumbe hai kama vile kuwapatia viumbe hai mwanga, joto na vitamini D.

### 2.2.2 Swali la 12: Ukombozi wa Bara la Afrika

Swali la 12 lilitoka katika mada ya *Ukombozi wa Bara la Afrika* na lilimtaka mtahiniwa atumie hoja tano kueleza mambo mbalimbali yaliyochochea harakati za kupigania Uhuru ndani ya nchi za Afrika mara baada ya Vita kuu ya Pili ya Dunia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,343 (100%) ambapo watahiniwa 685 (15.7%) walikuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa 2,008 (46.1%) walikuwa na ufaulu

wastani na watahiniwa 1,660 (38.1%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na. 12 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali 12.




**Chati Na.12:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 12.*

Uchambuzi wa takwimu katika swali hili unaonesha kuwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu *Ukombozi wa Bara la Afrika na walielewa* kwa ufasaha mahitaji ya swali. Pia, majibu ya watahiniwa yalidhihirisha kuwa, mada ya Ukombozi wa Bara la Afrika ilieleweka vizuri kwa wanachuo wengi wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo Na.12.1 ni mfano wa sampuli ya majibu yaliyo sahihi ya swali la 12.

12 vita kuu ya pili ya dunia; ni moja kati ya vita kubwa zilizotokea duniani mnamo mwaka 1939 hadi mnamo mwaka 1945 katika nchi za ulaya vita hii ilitokana na sababu mbalimbali zilizotokea katika Bara la ulaya ikiwemo sababu ya anguko la kiuchumi katika baadhi ya nchi za ulaya

zifuatazo ni sababu za harakati za kupigania uhuru katika nchi za Afrika zilizotokea baada ya vita kuu ya pili ya dunia

Kufanyishwa kazi katika mashamba ya wakoloni; Baada ya vita kuu ya pili ya dunia makoloni mengi ya ulaya yaliwafanyisha kazi za mashamba waafrika kwa muda mwingi ili wao waweze kufidia fedha zilizotumika na kupotea vita hivyo vilivyofanyika katika mataifa yao huko ulaya

Kupiga kutozwa kodi, pia utozwaji wa kodi ulipelekea nchi nyingi za Kiafrika kuanzisha mapambano dhidi za utawala wa kikoloni watu wa Afrika waliamua kuanzisha mapambano ili waweze kutetea haki zao. Waafrika walipewa ujira mdogo ambapo Haukuweza kuwasaidia kutimiza mahitaji yao wali tumia ujira huo mdogo katika kulipa kodi kwa mfano "kodi ya kichwa" na "kodi ya matiti"

Mafunzo waliyoyapata waafrika kutoka kwenye vita kuu ya kwanza ya dunia; katika vita kuu ya kwanza ya dunia kuna baadhi ya watu wa Afrika walishiriki katika vita hiyo hivyo iliwasaidia kupata ujuzi juu ya vita baada ya kupata ujuzi huo waafrika waliopata nafasi ya kurudi katika sehemu zao baada ya vita waliendo kuwaelekeza juu ya vita vilivyo kuwa kwa waafrika ambao hawakushiriki na baada ya hapo waliamua kuanzisha mapambano mbalimbali

12 Cont.

kwenye makoloni huika kwa mfano vita ya maji maji ilifanyika Tanganyika mnamo mwaka 1905 hadi mwaka 1907 huko kusini mwa Tanganyika

Kupinga unyonyaji; Unyonyaji wa wakoloni pia ulipelekea jamii nyingi za kiafrika kuanzisha harakati za kupigania uhuru baada ya vita kuu ya pili ya dunia. Baada ya waafrika kuona wananyanyasika katika maeneo yao. kwa mfano waafrika walipata elimu ya chini kabisa ili kusudi elimu hiyo iwasaidie waafrika kufanya kazi za wakoloni katika mashamba yao kwa kujua kusoma, kuhesabu na kuandika kwa sababu mtu akiweza kuhesabu ataweza kukufanya kazi

Kupinga kunyang'anywa ardhi zao zenye rutuba; kwa kuwa makoloni mengi yaliyokuja katika bara la Afrika walikuwa na uhitaji wa malighafi ili waweze kuzalisha bidhaa kwenye viwanda vyao hivyo walihitaji ardhi yenye rutuba ili waweze kuzalisha mazao yatakayowapatia malighafi kwa ajili ya viwanda vyao huko ulaya. hivyo tabia hizo waafrika hawakupendana kuamua kupigania uhuru wao.

Hivyo basi; kila taifa linapaswa kupigania haki za binadamu na kila taifa linapaswa kujiendeleza lenyewe katika nyanja ya utamaduni, siasa, uchumi na kijamii hivyo si vizuri mataifa ya ulaya kutawala mataifa mengine kwa kigezo chochote kile

**Kielelezo Na.12.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 12

Katika kielelezo Na.12.1, mtahiniwa alielewa matakwa ya swali na alikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Ukombozi wa Bara la Afrika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walitoa hoja bila kutoa maelezo vizuri na pia baadhi ya hoja kutokuwa na mashiko kulingana na matakwa ya swali. Baadhi ya watahiniwa

walishindwa kutoa utangulizi mzuri na hitimisho lililowiana na hoja walizotoa hivyo, kufanya ufaulu kuwa wa wastani.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walikosa maarifa juu ya mmada husika hivyo, kueleza mambo ambayo hayana uhusiano na swali, kama vile, *hali ya hewa nzuri, baadhi ya nchi kuwa chini ya baraza la udhamini la umoja wa Mataifa, biashara ya utumwa, kuweza kujitoa katika ujamaa* na *katiba za nchi husika*. Hoja hizo ni ishara tosha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika na hawakuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na.12.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 12.

**12** Kwa Kutumia hoja tano Mambo yaliyochochea harakati za Kupigania uhuru ndani ya nchi hizo. KTK Kipindi hicho.


Vita ya pili ya dunia: Hii ni vita ambayo vilipiganwa baina ya nchi mbili ambazo ni Waingereza na wajerumani mwaka 1937 - 1945 na Kiongozi wao haitwaye Kinjekitile ngwale.

Yafuatayo ni mambo yaliyochochea harakati za Kupigania uhuru ndani ya nchi hizo Katika Kipindi hicho

Kuwepo Kwa maeneo ya uwekezaji: Hili ni jambo lililochochea Katika nchi hizo Kupigania uhuru walitaka wapate maeneo ya uwekezaji ili waweze Kufanya shughuli zao mbalimbali ndio maana wakaweza Kupigania uhuru.

Kupata ardhi yenye rutuba: hili ni jambo ambalo lilihamasisha nchi hizo mbili ziweze Kupigania uhuru Kwa sababu walitaka wapate ardhi yenye rutuba ili waweze Kuanzisha shughuli mbalimbali Kama Kilimo na pia Kujenga nyumba mbalimbali.

Kuanzisha Viwanda: Nchi hizo mbili baada ya Vita ya pili ya dunia walipigania uhuru ili Kuweza Kuanzisha viwanda mbalimbali ambavyo vingewasaidia Katika Kuanzisha bidhaa zao mbalimbali.



Kustopisha biashara za utumwa baada ya vita vya
pili vya dunia nchi hizo mbili walianuo Kupigani
a uhuru ili Kuweza Kustopisha biashara za utumw
a ambazo zilikuwa zinaendelea katika nchi hizo.
Kuanzisha biashara mbalimbali Baada ya vita ya
pili ya dunia nchi hizo mbili walipigania uhuru ili wa
were Kupata maeneo mazuri ya Kuweza Kuanzisha
biashara zao mbalimbali.
Hiyo basi mambo ambayo yalichochea harakati za
Kupigania uhuru ndani ya nchi hizo ni maeneo ya
uwekezaji ardhi yenye rutuba n.k.

**Kielelezo Na.12.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 12

Katika kielelezo Na.12.2, mtahiniwa alieleza sababu zilizowafanya wakoloni kuja Afrika badala ya kueleza mambo yaliyochochea harakati za kupigania uhuru katika nchi nyingi za Kiafrika baada ya Vita kuu ya Pili ya Dunia.


### 2.2.3 Swali la 13: Upimaji na Tathmini

Swali hili lilitoka katika mada ya Upimaji na Tathimini. Swali lilimtaka mtahiniwa atumie hoja tano kuchambua umuhimu wa kumbukumbu za upimaji katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 4,353 (100%) ambapo watahiniwa 5 (0.1%) walikuwa na ufaulu hafifu. Aidha, watahiniwa 45 (1.0%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 4,303 (98.9%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na.13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 13.





**Chati Na.13:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 13.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa waliokuwa na ufaulu mzuri walieleza kwa usahihi jinsi *kumbukumbu za Upimaji zinavyosaidia katika kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji*. Pia walieleza kumbukumbu za Upimaji *zinavyowawezesha wathibiti ubora katika kufuatilia utekelezaji wa Mitaala*. Vilevile, mada hii hufundishwa katika masomo mengi hivyo ilikuwa rahisi kwa watahiniwa kuhawilisha maarifa kutoka somo moja kwenda jingine. Kielelezo Na.13.1 ni Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 13


13

Upimaji - Ni kitendo cha kutafuta ni kwanamna gani mwanafunzi ameweza kuelewa juu ya jambo fulani katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji huweza kufanywa kwa njia mbalimbali kama vile upi mazoezi, majaribio na mitihani. hivyo kumbukumbu za upimaji katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la jiografia ni ni muhimu sana. Ufuatao ni baadhi ya umuhimu wa kumbukumbu za upimaji katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la jiografia. nao ni:

Husaidia mwalimu kubaini changamoto za ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu ana potumia kumbukumbu za upimaji humsaidia katika kubaini changamoto mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji.





**Kielelezo Na.13.1:** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 13.

Kielelezo Na.13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la 13. Mtahiniwa alikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Upimaji na Tathimini kwani alielewa vizuri matakwa ya swali kwa kuwa alieleza kwa ufasaha umuhimu wa kumbukumbu za upimaji katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia.

Hata hivyo, watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani walishindwa kufuata maelekezo ya swali kwani baadhi yao walitoa tu sababu bila kutoa maelezo na wengine walitoa majibu yasiyoendana kabisa na matakwa ya swali.

Watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kwenye mada iliyotahiniwa. Pia, baadhi ya watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa hao walionekana kutokuwa na maarifa kabisa kwani walieleza mambo ambayo hayana uhusiano na swali na hivyo kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile; *humsaidia mwanafunzi kuwa msafi*. Kielelezo Na.13.2 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 13.

13 Upimaji: Ni mupangilio au mutekeo amba
o upata mwalimu katikamuchakato mzima
wa kujua maendeleo ya wanafunzi kati
ka ufundishaji na ujifunzaji
Umusaidia mwalimu kutambua changa
moto za wanafunzi
Kutumia kumbukumbu za ufundish
aji: mwalimu au mtarumu yoyote an
aweza kutumia kumbukumbu zake
kwa ajiri ya kutikisha ujumbe kwa
wale wanao musikiliza na kuwez
a kuelewelza.
Kutumia ujuzi, marifa: mtu anaweza
kutumia ujuzi au marifa kupitia
kumbukumbu zake kuweza kuwa
fundisha wengine au kuwapa mae
lekezo kuusiana na uelewa alio
nao kwa ajili ya kufundisha
na kujifunza.
Uandaaji wa ujifunzaji: mwalimu
anatakiwa kuanda kile anachota
rajia kufundisha na kujifunzia
katika somo la jiografia kwa
ajiri ya kuelimisha wengine.
Kuendeleza viwango vya kuelewa:
Utunzaji wa kumbukumbu wa umu
himu wa upimaji unasaidia,
watu watarumu mbalimbali kwa
ajili ya kuendeleza viwango vya
o vya kuelewa na kuweza ku
kutumia kwa ajili ya kufundi
shia na kujifunzia.


| 13 Cont. | Kuwa na ujuzi wa na uelewa wa kutumi |
|---|---|
| | a zana za kufundishia na kujitumia: wa |
| | atakiwa kuwa na kumbukumbu kuusuana |
| | na na zana na namna na kuweza |
| | kuzitumia katika ufundishaji na ujifu |
| | nzaji . |

**Kielelezo Na.13.2.** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 13

Katika kielelezo Na.13.2, mtahiniwa hakuelewa dhana na mahitaji ya swali kwani alichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi pia, aliorodhesha hoja chache tofauti na matakwa ya swali na hivyo kusababisha ufaulu hafifu.

### 2.2.4 Swali la 14: Kujiandaa kwa ajili ya Kufundisha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Kujiandaa kwa ajili ya Kufundisha.* Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja tano kueleza udhaifu wa usemi kwamba "kwa kuwa Maliyamungu ni mwalimu mzoefu amefundisha somo la historia kwa miaka ishirini na tano hivyo hahitaji andalio la somo kwa sababu yeye ana uzoefu". Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,343 (100%) ambapo watahiniwa 26 (0.6%) walikuwa na ufaulu hafifu. Pia, watahiniwa 4,077 (93.7%) walikuwa na ufaulu wa wastani na watahiniwa 250 (5.7%) walikuwa na ufaulu mzuri. Chati Na. 14 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa swali la 14.




**Chati Na.14:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila kundi la ufaulu kwa swali la 14.*

Uchambuzi wa ufaulu, katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa wastani wengi walitoa hoja ambazo maelezo yake yalikuwa hayajitoshelezi. Aidha baadhi ya watahiniwa walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo kupata ufaulu wa wastani.

Aidha, watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Kujiandaa kwa ajili ya Kufundisha na waliweza kubaini matakwa ya swali. Watahiniwa katika kundi hilo walibainisha umuhimu wa andalio la somo katika ufundishaji kwa kuwa, ni mojawapo ya vifaa muhimu vya mtaala ambavyo watahiniwa wanavitumia wakati wa mazoezi ya kufundisha kwa vitendo.

14


Andalio la somo: ni mpango kazi wa m
da mfupi ambao humsaidia mwalimu
kufundisha ndani ya kipindi cha dakika
40 au 80. andalio la somo huweza kuan
daliwa ndani ya kipindi cha dakika ar
obaini au themanini kwasababu ni mp
ango kazi wa mda mfupi na andalio
la somo huandaliwa na mwalimu kulin
gana na mada aliyokusudia ili kuweza ku
rahisisha ufundishaji wake na ujifunzaji w
ake. na bila andalio la somo ni vigumu sa
na mwalimu kufundisha somo lake kwa
sababu andalio la somo ndicho kiini ch
a somo husika. Zifuatazo ni sa athari za
mwalimu kufundisha bila andalio la som
o lake

Ni rahisi mwalimu kutoka nje ya m
ada. Mwalimu asipoandaa andalio la somo
ni rahisi sana. kutoka nje ya mada kw
asababu hajaandaa andalio la somo lake
na hivyo andalio la somo lina umuhim
u mkubwa sana kwa mwalimu kwani
humsaidia mwalimu asitoke nje ya ma
da na hivyo mwalimu anapoandaa and
alio la somo inamsaidia asitoke nje ya m
ada hivyo hivyo inampelekea mwalimu
kutoka nje ya mada

Mwalimu kushindwa kufundisha kwa mt
iririko; pia mwalimu asipoandaa andalio la
somo ni vigumu kufundisha kwa mtiririk
o maalumu kwasababu hajaandaa and
alio la somo lake na hivyo mwalimu

14 Cont. anaweza kufundisha bila kufuata mtiririko maa
lumu hivyo basi ni vyema mwalimu akaa
ndaa andalio la somo kabla ya kuingia d
arasani kwake ili kuweza kufundisha kw
a urahisi

Mwalimu kushindwa kufikia lengo mahsu
si; mwalimu asipoandaa andalio la somo
lake huweza kushindwa kufikia lengo alilo
kusudia kwasababu hana andalio la somo
na andalio la somo ni muhimu sana k
wa mwalimu kwani humsaidia mwalim
u kuweza kufikia lengo mahsusi hivyo basi
mwalimu asipoandaa andalio la somo ni vig
umu kufikia lengo mahususi



Mwalimu kushindwa kufundisha kwa kujiamini. Pia ni vyema kuandaa andalio la somo kwa mwalimu kwani humsaidia mwalimu kufundisha kwa kujiamini na hivyo ni muhimu mwalimu kuandaa andalio la somo lake ili aweze kufundisha kwa kujiamini hivyo basi mwalimu kushindwa kufundisha kwa kujiamini ni moja wapo ya athari za mwalimu kutokuandaa andalio la somo wakati wa ufundishaji.

Mwalimu kutumia muda mrefu wakati wa ufundishaji; kwa mfano, andalio la somo linasema ndani ya kipindi cha dakika arobaini mwanafunzi aweze kueleza umuhimu wa kutunza mazingira lakini mwalimu kwa kutokuandaa andalio la somo huweza kufundisha kwa lazima na inapelekea mwalimu kuchukia somo

14 Cont.


Hivyo basi, andalio la somo lina umuhimu mkubwa sana kwa mwalimu kwani humsaidia mwalimu kuweza kufundisha kwa mtiririko, humsaidia mwalimu kufundisha kwa kujiamini, humsaidia mwalimu kufikia lengo mahususi, humsaidia mwalimu kutumia muda,

**Kielelezo Na.14.1**: Sampuli ya majibu sahihi ya swali la 14

Katika kielelezo Na.14.1, mtahiniwa alielezea kwa usahihi umuhimu wa kuandaa andalio la somo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walikosa umakini katika kubainisha matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa kabisa kwani walieleza mambo ambayo hayana uhusiano na swali hivyo kupata ufaulu hafifu. Aidha, baadhi ya watahiniwa katika kundi hilo walichanganya majibu sahihi na ambayo

hayakuwa sahihi. Aidha baadhi ya watahiniwa waliweza kuelewa kiini cha swali lakini walitaja hoja zao bila maelezo ya kina kuhusu umuhimu wa andalio la somo. Halikadhalika, baadhi ya watahiniwa walitaja hoja pungufu ya zile zilizohitajika na wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho hivyo kupata ufaulu hafifu. Kilelelezo Na. 14.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 14


14 Andalio la somo; Ni mpango kazi wa muda mfupi anaotumia mwalimu wa kati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo husika kwa ndani ya kipindi kimoja.

Mwalimu kushindwa kufikia malengo yake.

Mwalimu kutojiamini wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo husika

Mwalimu kwende nje ya muda wakati wa ufundishaji na ujifunzaji

Mwalimu kutokuwa na mtiririko mzuri wa ufundishaji na ujifunzaji.

**Kielelezo Na.14.2**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya swali la 14.

Katika kielelezo Na.14.2, mtahiniwa alikuwa na maarifa kuhusu umuhimu wa andalio la somo lakini alitoa hoja chache na alishindwa kuzielezea.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada unaonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali za mtihani wa Maarifa ya Jamii ulikuwa mzuri. Mada zilizotahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii zilikuwa kumi na moja. Kati ya hizo mada kumi (10) zilikuwa na ufaulu mzuri. Mada hizo ni: *Upimaji na Tathimini* (99.89%), *Kujiandaa kwa ajili ya Kufundisha* (99.40%), Stadi Sahili na *Tata za Picha na Ramani* (98.60%), *Ufundishaji wa Mada za Somo la Historia* (97.11%), *Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika* (95.22%), *Maandalizi ya Kufundisha na Kujifunza* (89.55%), *Ukombozi wa Bara la Afrika* (84.26%), *Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika Zanzibar na kwingineko Afrika* (83.37%), *Sayari Dunia* (84.06%) *Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na kiuchumi katika Afrika Huru* (72.17%). Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa ufaulu ulikuwa wa wastani

katika mada ya *Nchi yetu Tanzania* (41. 81%). Hapakuwa na mada ambayo ufaulu wake ulikuwa hafifu.

Aidha uchambuzi zaidi ulifanyika ili kubaini mwenendo wa ufaulu katika mada hizo ikilinganishwa na mwaka 2022. Uchambuzi huo ulibaini kuwa, ufaulu umeendelea kuwa mzuri katika mada za: *Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Historia, Mabadiliko ya Kijami, Kisiasa na kiuchumi katika Afrika Huru, Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Wakoloni na vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika Zanzibar na kwingineko Afrika.* Vilevile mada ya *Nchi yetu Tanzania* imeendelea kuwa na ufaulu wa wastani kama ilivyokuwa mwaka 2022.

Jumla ya watahiniwa 4,353 walifanya mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii ambapo asilimia 100 walifaulu. Kiwango hiki cha ufaulu kimeongezaka kwa asilimia 0.03 ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo asilimia 99.97 ya watahiniwa walifaulu.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, uchambuzi wa taarifa hii umeonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii 2023 ni mzuri ikilinganishwa na ufaulu katika mwaka 2022. Hii ni ishara kuwa wakufunzi na wadau mbalimbali wanachukua hatua stahiki katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Jiografia na Historia.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua ufaulu katika mada ya *Nchi yetu Tanzania* ambayo imeendelea kuwa na ufaulu wa wastani (41.81%), yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Wakufunzi watumie mbinu shirikishi ili kuwawezesha walimu tarajali kuhusianisha vipengele muhimu vya umbali katika Dunia, na tabianchi badala ya wakitumia tufe na ramani pekee, kwani hoja hii imeonekana kuwa tatizo kwa watahiniwa wengi.

(b) Walimu tarajali wapewe kazi mradi kuhusu tabianchi na hali ya hewa ili kuwajengea uelewa wa hali ya hewa na namna kila kipengele cha hali hewa kinavyoweza kuwa na tabianchi tofauti.

(c) Wakufunzi watumie mazingira halisi ikiwemo njia ya ziara ili kuwaongezea maarifa na kuwapa walimu tarajali kumbukumbu ya kudumu.

**Kiambatisho cha Pekee**

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA MAARIFA YAJAMII 2023

| | | Ufaulu 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Mada** | **Namba ya Swali** | **Asilimia ya Watahiniwa wenye ufaulu wa 40% au zaidi** | **Wastani wa wathiniwa wenye aslilimia 40 au zaidi** | **Maoni** |
| 1. | Upimaji na Tathimini | 13 | 99.89 | 99.89 | Vizuri |
| 2. | Kujiandaa kwa ajili ya kufundisha | 14 | 99.40 | 99.40 | Vizuri |
| 3. | Stadi Sahili za Picha na Ramani | 2 | 98.60 | 98.60 | Vizuri |
| 4. | Ufundishaji wa Mada za Somo la Historia | 7 | 97.11 | 97.11 | Vizuri |
| 5. | Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika | 5 | 95.22 | 95.22 | Vizuri |
| 6. | Maandalizi ya Kufundisha na Kujifunza | 9 | 89.55 | 89.55 | Vizuri |
| 7. | Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika | 6 | 84.26 | 84.26 | Vizuri |
| 8. | Ukombozi wa Bara la Afrika | 12 | 84.06 | 84.06 | Vizuri |
| 9. | Sayari Dunia | 1 | 68.22 | 83.37 | Vizuri |
| | | 11 | 99.91 | | |
| 10. | Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa,na Kiuchumi Katika Afrika Huru | 8 | 68.64 | 72,17 | Vizuri |
| | | 10 | 75.37 | | |
| 11. | Nchi yetu Tanzania | 3 | 37.28 | 41.81 | Wastani |
| | | 4 | 46.34 | | |